FUNZO LA 53

1. Mtu aliyepooza aliweza kujiponya?
-La.

2. Je, Marafiki wa yule aliyepooza waliweza kumponya?
-La.

3. Je, kuna daktari yeyote aliyeweza kumponya yule aliyepooza?
-La.

4. Je, wanaume walimleta kwa nani mtu aliyepooza?
-Kwa Yesu.

5. Ni nani pekee aliyeweza kumponya yule aliyepooza?
-Yesu.

6. Je, kuna mtu yeyote anayeweza kusamehe dhambi?
-La.

7. Je, kuhani anaweza kusamehe dhambi?
-La.

8. Kwa nini Yesu aliweza kuwasamehe watu dhambi zao?
-Kwa sababu Yesu ni Mungu.

9. Kwa nini Yesu alikuwa na mamlaka ya kusamehe dhambi?
-Kwa sababu Yesu ni Mungu.



10. Jina la pili la Lawi lilikuwa lipi?
-Mathayo.

11. Ni kazi gani Mathayo alifanya wakati Yesu alimwita?
-Mathayo alikuwa mtoza ushuru.
-Mathayo alikusanya ushuru kwa niaba ya Warumi, akichukua ushuru kutoka kwa watu wake, Wayahudi.

12. Yesu aliwaambia Mafarisayo kuwa watu wenye afya hawahitaji daktari, lakini wagonjwa wanahitaji. Yesu alimaanisha nini?
-Yesu alimaanisha kwamba hakuja kuwaokoa watu ambao hawajui kuwa wao ni wagonjwa.

13. Ni nani ambaye Yesu alikuja kuokoa?
-Yesu alikuja kuokoa watu tu ambao wanajua kuwa wamemkosea Mungu, na kwamba ni Mungu tu ndiye anayeweza kuwaokoa.

-Siku moja, baadhi ya Mafarisayo na walimu wa sheria waliuliza kuona ishara ya miujiza kutoka kwa Yesu.

Tusome Mathayo 12:38

38-Hapo baadhi ya waandishi na Mafarisayo wakamjibu, wakasema, Mwalimu, twataka kuona ishara kwako.

-Badala ya kuamini Neno la Mungu, Mafarisayo na walimu wa sheria walitaka kuona nini?

-Walitaka kuona ishara ya miujiza.

-Kwa nini Mafarisayo na walimu wa sheria waliuliza kuona ishara ya miujiza?

-Je, hawakuona au kusikia kwamba Yesu anatoa pepo kutoka kwa watu?
-Ndiyo.

-Waliona.

-Je, walikuwa hawajaona au kusikia kuwa Yesu alimponya mtu mwenye ukoma?
-Ndiyo.

-Waliona.

-Je, hawakuona au kusikia Yesu akimponya yule mtu aliyepooza?
-Ndiyo.

-Waliona.

-Je, hawakuona au kusikia kwamba Yesu aliwaponya wote waliomjia?
-Ndiyo.

-Waliona.

-Kwa nini basi Mafarisayo na waalimu wa sheria waliuliza



kuona ishara zaidi za miujiza?

-Kwa sababu hawakuamini kwamba Yesu alikuwa Mungu Mwokozi.

-Badala ya kumwamini Yesu, Mafarisayo na walimu wa sheria walitaka tu kuona ishara za miujiza.

-Badala ya kuamini Neno la Mungu, Mafarisayo na waalimu wa sheria walitaka tu kuona ishara za miujiza.

-Unakumbuka jinsi Mungu aliwaonyesha Waisraeli ishara nyingi za miujiza, na bado hawakuamini?

-Mungu alituma mapigo kumi kwa Farao na Wamisri, na Waisraeli bado hawakuamini.

-Mungu alimzamisha Farao na jeshi lake katika Bahari ya Shamu, na Waisraeli bado hawakuamini.

-Mungu alituma kware na mana kwa Waisraeli jangwani, na bado hawakuamini.

-Badala ya kumwamini Yesu, watu wengi wanataka tu kuona ishara za miujiza.

-Je, kuona ishara za miujiza kutatuokoa?
-La.

-Kumuamini tu Yesu Mwokozi ndiko kutatuokoa.

-Ikiwa tunasema kwamba tutamwamini Yesu tu wakati tutakapoona ishara ya miujiza, basi tunasema nini?

-Kwamba Yesu ni mwongo.

-Ikiwa tunasema kwamba tutaamini kuwa Neno la Mungu ni la kweli tu tunapoona ishara ya miujiza, basi tunasema nini?

-Kwamba Neno la Mungu ni uwongo.

-Je, Yesu aliwajibu nini Mafarisayo na walimu wa sheria?

Tusome Mathayo 12:39

39-Akajibu, akawaambia, Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara, wala hakitapewa ishara, ila ishara ya nabii Yona.

-Yesu alisema nini?

-Yesu alisema kuwa ni watu waovu tu na wazinifu wanaouliza ishara.

-Nini ilikuwa ishara pekee ambayo Yesu alisema atawapa watu?

-Ishara ya Yona.

-Nini ilikuwa ishara ya Yona?



Tusome Matayo 12:40

40-Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.

-Nini ilikuwa ishara ya Yona?

-Kama vile Yona alikuwa ndani ya tumbo la samaki mkubwa kwa siku tatu na usiku tatu, kwa hivyo Yesu pia atakuwa ndani ya tumbo la dunia kwa siku tatu na usiku tatu.

-Kama vile Mungu alimtoa Yona ndani ya tumbo la samaki mkubwa baada ya siku tatu na usiku tatu, kwa hivyo Mungu pia atamtoa Yesu ndani ya tumbo la dunia baada ya siku tatu na mchana.

-Yesu alikuwa akiwaambia Mafarisayo na walimu wa sheria kwamba ishara ya Yona ilikuwa ishara ya kwamba Yeye ni Mungu Mwokozi.

-Je, Yesu alisema nini kwa Mafarisayo na walimu wa sheria?

Tusome Mathayo 12:41

41-Watu wa Ninawi watasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, nao watawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; na hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona.

-Yona alikwenda kwa watu waovu wa Ninawi na kuwaambia watubu dhambi zao la sivyo Mungu atawaadhibu.

-Watu wa Ninawi walifanya nini?

-Walisikiliza Neno la Mungu ambalo Yona alifundisha, na kutubu dhambi zao.

-Je, watu wa Ninawi walijua ahadi za Mungu ambazo alimpa Ibrahamu, Isaka, na Yakobo?
-La.

-Je, watu wa Ninawi walijua amri za Mungu alizompa Musa?
-La.

-Je, watu wa Ninawi walijua ishara zote za miujiza ambazo Mungu aliwafanyia Waisraeli?
-La.

-Ijapokuwa watu wa Ninawi hawakujua haya, bado walitubu dhambi zao wakati Yona aliwafundisha.

-Sasa, aliye mkuu kuliko Yona alikuwa akiwafundisha watu kutubu.

-Ni nani aliye Mkuu kuliko Yona?

-Yesu, Mungu Mwokozi.

-Ni jinsi gani Yesu alikuwa mkuu kuliko Yona?



-Yona alikuwa mtu tu, lakini Yesu alikuwa mtu kamili na Mungu kamili.

-Ijapokuwa Yesu alikuwa Mungu Mwokozi na Yona alikuwa mtu tu, Wayahudi bado walikataa kuamini.

-Ijapokuwa mafundisho ya Yesu yalikuwa makubwa kuliko ya Yona, Wayahudi bado walikataa kuamini.

-Ijapokuwa Yesu alifanya ishara nyingi za miujiza ambazo Yona hakuweza kufanya, Wayahudi bado walikataa kuamini.

-Kwa nini Yesu alisema kuwa Wayahudi walikuwa waovu zaidi kuliko watu wa Ninawi?

-Kwa sababu watu wa Ninawi walitubu kwa mafundisho ya Yona, na Wayahudi hawakutubu kwa mafundisho ya Yesu, Mungu Mwokozi.

-Ijapokuwa Yesu aliwafundisha Wayahudi kutubu na kufanya ishara nyingi za miujiza, Wayahudi bado walikataa kuamini kwamba Yeye alikuwa Mungu Mwokozi.